

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

ISO 9001:2015 CERTIFIED



TAARIFA KWA UMMA

UPATIKANAJI WA HUDUMA YA INTANETI NCHINI

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inapenda kuutaarifu umma kuwa kuanzia tarehe 12 Mei 2024 mnamo majira ya saa tano asubuhi, kumekuwa na tatizo la upatikanaji wa huduma ya intaneti nchini.

Taarifa za awali zimeonesha kuwa tatizo hilo limesababishwa na hitilafu kwenye mkongo wa mawasiliano wa baharini wa kampuni za SEACOM na EASSY kati ya Msumbiji na Afrika ya Kusini.

Tatizo hilo limepelekea huduma za intaneti kuwa hafifu nchi nzima. Hata hivyo, jitihada za haraka zimefanyika na zinaendelea kuchukuliwa na watoa huduma wote ikiwemo kutumia njia mbadala ambapo huduma zilianza kurejea kuanzia jana tarehe 12 Mei 2024 kwa baadhi ya watoa huduma.

Aidha, upatikanaji wa huduma ya intaneti kwa kutumia njia mbadala utaendelea kuimarika kwa kadiri uimarishaji wa njia hizo kwa kila mtoa huduma unavyoendelea. TCRA inaendelea kufuatilia kwa karibu suala hili na taarifa za upatikanaji wa huduma ya intaneti zitaendelea kutolewa na kila mtoa huduma wa intaneti kulingana na jitihada zinazoendelea.

Imetolewa Tarehe **13 Mei 2024**.

Dkt. Jabiri K. Bakari
MKURUGENZI MKUU

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.

Simu: +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Nukushi: +255 22 2412009-10

Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz